REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THIRD ASSEMBLY-THIRD SESSION

THE HANSARD

Wednesday, 6th March 2024

The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 2:30 p.m.

[The Temporary Speaker (Hon. Stephen) in the Chair]

QUORUM

QUORUM CALL AT COMMENCEMENT OF SITTING

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Kaeni waheshimiwa. Bw. Clerk, tuko na idadi kamili ambayo inatuwezesha kuendelea na Bunge hili saa hii.

Clerk at-the-Table: Mr. Speaker, we do not have quorum.

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Sasa, ningeomba kengele ipigwe kwa dakika kumi.

(The Quorum Bell was rung for ten minutes)

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Je, Bw. Clerk, kuna idadi kamili ya Waheshimiwa ambayo tunaweza tukaendeleza Bunge?

Clerk at-the-Table: Mr. Speaker, we have a quorum.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

MOTION

THANKS FOR THE SECOND SENATORIAL ADDRESS – THIRD ASSEMBLY 2024

THAT, the thanks of the County Assembly be recorded for the exposition of public policy contained in the Address of the Senator (Rtd.) Justice Steward Madzayo CBS, given on Thursday, 22nd February 2024.

(Hon. Ibrahim on 5.03.2024)

(Resumption of Debate interrupted on 5.03.2024)

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Asante sana. Twende katika Hoja ya kwanza. Kama vile mwajua, tulitembelewa na Seneta wetu Madzayo, akaja akatupatia hotuba tarehe Ishirini na mbili (22) ya mwezi wa Pili mwaka huu na jana tulikuwa na Hoja ya kujadili ile hotuba yake asubuhi na tukawa na tena saa nane jana.

Vile vile, leo hii bado tunaendelea kujadili ile hotuba ya mheshimiwa Seneta wetu. Lakini wale ambao jana walipata nafasi ya kutoa Hoja zao ningewaomba watulie kidogo ili wale ambao hawakupata nafasi ya kutoa hotuba zao basi wako huru na nafasi ni yao waanze kutoa. Karibuni waheshimiwa. Waheshimiwa, yule ambaye anataka kujadili ile Hoja, unaweza kuweka *request* yako na upewe nafasi uendelee kujadili ile Hoja ambayo tulikuwa tunaendelea nayo jana. Mheshmiwa Grace Mwangi.

Hon. (Ms.) Radhia: Asante, mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia changizo zangu kulingana na Hotuba ya mheshimiwa Seneta wetu Madzayo. Jina langu ni Radhia Ali Omar na natumia kadi ya mwenzangu, yangu yasemekana haijaonekana. Nataka nimkumbushe mheshimiwa Madzayo ya kwamba kuna kitabu chaitwa 'Maji Maji Rebellion' tulikipitia wakati tulikuwa shule. Hicho kitabu kinasema mtu huzaa neno na hilo neno likawa kubwa kushinda mwenyewe aliyelizaa.

Kwa hivyo, ni kumjulisha mheshimiwa Madzayo kwamba wakati akizungumza hotuba yake awe na makini analoongelea; akumbuke litakuwa na mambo mengi huko nje kwa wasiojua na hata wanaojua na italeta maana nyengine kulingana na Kaunti yetu ya Kilifi wakati sivyo mambo yalivyo. Kisa kifupi ni hiyo "Maji Maji Rebellion" yeye alitangaza. Nikiwakumbusha wenzangu kwamba maji maji ukipaka maji hata bunduki pia haifanya nini, haitapita. Kwa hivyo, watu hilo neno likawakumba kushinda yeye mwenyewe aliyelizaa lile neno.

Ndio mfano wa mheshimiwa Madzayo kwamba yeye ataongea yatakwisha kwake mdomoni lakini, watakaochukua watachukua watatafsiri ki vingine wanavyotaka wao wenyewe. Kwa hivyo, ni muhimu kama mheshimiwa *Majority* alivyosema na Hassan kwamba na yoyote anayekuja iwe ni kama sheria iwepo kwanza katika hili Bunge letu la Kilifi tuikague ile hotuba. Tukiona ile hotuba iko sawa tuipitishe na mwenye kuja kuongea aje aongee na kama tukiona ile hotuba haiko sawa ni lazima tuwekane sawa na kazi iendelee kwa sababu mambo mengine ni kama kuvunjiana heshima ama kukoseana uaminifu na sote ni viongozi na sote twahitaji kura miaka ijayo. Mimi wa kwanza naomba kiti cha Shella *Ward*, natangaza rasmi, sawa.

(Laughter)

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kwa hivyo, mheshimiwa Spika, inakuwa si vyema kama sifa zetu kule nyanjani zitakuwa si nzuri; itakuwa ni Bunge zima si mtu mmoja ambaye ameharibu jina lake na itakuwa sote tumeharibu kwa sababu sote itakuwa hatukuona yale makosa mpaka Seneta akatoka kule akaja hapa Kilifi na akaweza kugundua yale makosa wakati sivyo vile vilivyo.

Kwa hivyo, naomba kama ombi hotuba yoyote itakayokuja hapa kwanza ichunguzwe ikionekana yatufaa iendelezwe na kama haitufai tusikubali sisi kama Wabunge wa Bunge la Kilifi kutoa nafasi ya mtu aje azungumze yale atakayoona kwa roho yake kama ni kisiasa kama ni kivipi lakini sote ni waheshimiwa na lazima pia sisi tuheshimike. Asante.

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Asante sana, mheshimiwa. Umetukumbusha historia ya mbali sana, 'Maji Maji Rebellion'. Mheshimiwa Edward Ziro, karibu katika ukumbi ujadili kuhusu Hoja ya mheshimiwa Madzayo.

Hon. Ziro: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi hii mimi pia niweze kutoa hisia zangu kulingana na hotuba ya Seneta wa Kilifi Kaunti. Nafikiri hotuba hii, Bw. Madzayo aliongea mengi na yale yaliweza kufurahisha wana Kilifi. Lakini cha kushangaza mheshimiwa Spika, mbali na yale yote ambayo Seneta aliweza kutueleza kwanza kabisa nikinukuu ukurasa wa tano namba kumi na mbili; Seneta alituambia wazi kwamba yeye hawezi kutekeleza usimamizi wa kaunti kwa sababu hajapewa fedha, hawezi kutekeleza majukumu yake kama Senata katika Jimbo la Kilifi kwa sababu hajapewa zile fedha sahihi ambazo zinafaa yeye kusimamia yale majukumu yake.

Na pia hapa chini, katika ukurasa 15 ametuma Wajumbe wa Kilifi kwamba waweze kujua majukumu yao. Sasa swali ambalo nitamuuliza mheshimiwa Seneta ni kwamba alijuaje kama yeye hafanyi majukumu yake kwa sababu hakuwa amepewa zile fedha za ule mfuko wake aliokuwa ameitisha za *oversight fund*? Alijuaje kwamba Kilifi kuna ufisadi? Alijuaje kwamba hapa Kilifi wanafunzi hawasomi? Kwa hivyo, nafikiri hii hotuba yake haikuwa mahali ambako inafaa. Nataka tumkumbushe kwamba sisi kama wajumbe tumefanya majukumu yetu bila mfuko wowote wa fedha ambao tumeweza kuwekewa na yeye kama Seneta wetu anafaa awe anaweza kututetea ili kwamba sisi tuweze kupata ule mfuko.

Lakini sisi hatujalalamika na tumekuwa tukifanya majukumu yetu ndio maana umekuwa ukiona Mawaziri wakija wakijibu maswali katika Bunge hili. Nataka nimkumbushe mheshimiwa Seneta kwamba hapa kwetu Kilifi nafikiri baada ya kuchukua hatamu ya hii miaka mitano ya kwanza, tumeweza kwenda mbali sana kimaendeleo. Ikizingatiwa kwamba hasa kitengo cha Afya saa hii tuko kati ya namba tano na namba kumi (5-10) katika Kenya nzima kimaendeleo; hayo si ni maendeleo? Sasa akija akitwambia kwamba Kilifi haiendelei kwa sababu kuna ufisadi hilo ni jambo ambalo laweza kutamausha kila mmoja. Akituambia kwamba kuna ufisadi katika upande wa elimu nafikiri kwa mara ya kwanza tumeweza kupeleka *National* zaidi ya watoto elfu mbili (2,000). Ni jambo ambalo halijawai fanyika katika Jimbo letu hili la Kilifi tangu ugatuzi uanze. Sasa badala ya kutupongeza, anaturudisha nyuma tena na kutuambia kwamba kuna vitu fulani ambavyo haviendelei.

Pia mimi ninaungana na wenzangu ya kwamba kabla hajakuja kutueleza yale ambayo yuko nayo tena hapa Bungeni, itabidi kwanza tuangalie ile hotuba yake na kama itakuwa haitufai, basi itakuwa haina haja tukae ndani hapa ya hili Bunge tukufu tusikize uongo ambao utaleta uoga katika wananchi watukufu wa Jimbo hili letu la Kilifi. Asante, Bw. Spika.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Asante, mheshimiwa Edward Ziro. Ni ukweli kabisa, ukiongea mambo ya afya Kilifi tuko kweli namba tano na tunaendelea vizuri. Hon. Twaher.

Hon. Twaher: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa hii nafasi. Tuko nambari 10 kwa mambo ya afya na nambari moja Pwani. *That is for record purpose.*

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Umefanya vizuri kunirekebisha hapo.

Hon. Twaher: Mheshimiwa Spika, asante kwa fursa hii tena. Niko na furaha kwamba tumepata kuelewa kwamba baadhi ya viongozi ambao kwamba tunawaheshimu na tunawapatia fursa ili kuenda kutuwakilisha katika nyumba za kitaifa, hawana ufahamu wa mambo yanayoendelea katika Kaunti. Ni muhimu sana Seneta wa Kilifi kupata ufahamu wa mambo ambayo yanaendelea katika Kaunti ya Kilifi kabla kuja kueleza mambo ambayo hayana ukweli.

Hii ni kwa sababu, mambo mengi katika hotuba ya Seneta wetu ni mambo ambayo ni ya dhana. Mambo ambayo hayana ukweli, akiambiwa athibitishe, hivi sasa mazungumzo aliyoyaleta yatamshinda. Siku zote mwenye kuongea jambo katika Nyumba ya Kisheria, kuweka kwa mabano wanasema *"the burden of proof"* inatoka kwa yule mtu ambaye kwamba ameleta Hoja yake katika Nyumba hii.

Haya mambo ambayo yamezungumzwa na Seneta wetu wa Jimbo la Kilifi ni mambo ambayo yanahuzunisha sana; hatukutarajia kuwa mtaalamu kama yeye atakuja kuzungumza maswala kama yale. Tuko na changamoto kubwa sana ya kisheria ambayo kwamba napenda kuiweka wazi kwa watu wetu wa Kilifi ambao hapa wajumbe wote wana masikitiko makubwa sana. Kwamba, kuna mkandarasi ambaye aliingia kwa makubaliano na Kaunti hii, kampuni ya *Raindrops*, na hiyo kampuni imefilisisha na imedhoofisha maendeleo ya Kaunti yetu ya Kilifi.

Kaunti yetu tumesimamisha makubaliano na wao, wakaenda kortini, leo mpaka hivi sasa tunagharamikia kampuni ambayo kwamba haitumikii Kaunti yetu ya Kilifi. Gharama ya shilingi milioni nne kila mwezi; hili ni jambo la kusikitisha sana. Tulifikiria Seneta atalizungumzia kwa sababu yeye amehudumu katika kitengo cha majaji na ni mtu mwenye tajriba kubwa ya mambo ya uanasheria. Tumetarajia atapeana ushirikiano mkubwa ili kuokoa rasilmali ya wananchi wa Kilifi lakini yeye kwa sababu ni mhusika mkuu… na ninaomba tena nirudie kwa sababu yeye ni mhusika mkuu, kwa sababu kipindi makubaliano yalivyowekwa ni kipindi yeye pia bado vile vile alikuwa ni Seneta wa Jimbo letu la Kilifi na makubaliano yale yaliwekwa na mpaka leo sisi tunaingia hasara.

Ni jambo ambalo linatutia uchungu sana na wananchi wanatarajia zile pesa zipeleke maendeleo katika shule zetu, hospitali zetu na katika kusaidia karo za wanafunzi na kusambaza maji mashinani. Hivi leo, pesa zinaingia kwenye mifuko ya mabwenyenye na sisi tunataka kujua yeye kama Seneta, maanake Ripoti imepelekwa wazi wazi, mimi nikikaa katika Kamati ya PIC/PAC *(Public Investments and Accounts Committee)* tulikwenda Seneti na tukapambana na Kamati ya PIC/PAC na Ripoti mheshimiwa Gavana aliiweka bayana kwamba sisi tuko na changamoto.

Tuko na changamoto ya pesa ambazo zinalipwa kampuni ambayo kwamba ni kinyume na sheria. Tunahitaji Bunge la Seneti liingilie swala kama hilo na mpaka leo limenyamaziwa; halijazungumzia hiyo Ripoti ya upande wa kule Seneti. Mpaka leo hatujajua hilo swala limezungumziwa vipi na pesa zetu bado zinalipa Raindrops. Ni swala la kisheria kwamba Bunge hili tumeliketia, tumelijadili na mkandarasi kila akiitwa katika hili Bunge ambapo Bunge hili liko na fursa ya kumuita anatoa sababu kuwa hiyo kesi iko kortini.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Sasa korti gani? Hivi leo sisi tunajisifu na tukiweka maringo kwamba tuko na Seneta ambaye ni *retired Judge* na hawezi kusaidia kuokoa Jimbo la Kiifi kuingia hasara. Anakuja kuweka hotuba ya uongo; maneno mengi ya uongo ambayo kwamba hayako sawa. Swala la kisheria lolote, ningependa kunukuu vile Kiongozi wa Wengi alivyosema. Swala la EACC *(Ethics and Anti-Corruption Commission)* kama ni swala linachunguzwa halijapata ithibati, huwezi kusimama nalo kwa msimamo wa msingi wa kusema kuna ufisadi.

Kitu chochote ambacho bado kiko katika uchunguzi, wacha uchunguzi ufanywe, mwenye amepatikana na hatia ashikwe apelekwe korokoroni ndio tutajua kweli kuna fulani alikuwa mfisadi. Gavana wetu amekuwa mstari wa mbele kupambana na maofisa ambao wanazembea kazini. Tumeshuhudia mabadiliko mara kwa mara kwa sababu tunataka utendakazi usonge mbele katika Jimbo letu la Kilifi. Ni swala la kuja mtu katika Bunge hili kutuunga mkono na kutupatia motisha na ruwaza zake kutuongeza msukumo na vipi tuta weza kusongeza Jimbo letu mbele.

Yeye anakuja kutuvunja moyo na kutuambia kwamba sisi tumezembea katika kazi zetu na sisi kila Kamati hapa inawajibikaji. Kamati ya Afya imezunguka katika hospitali zetu usiku, waheshimiwa hawa wamezunguka usiku wa manane, wakaacha familia zao kutembea katika hospitali zetu kuangalia vipi watu wetu wanapata huduma sawa ama si sawa na wakatengeneza Ripoti na imepelekwa kule ili mabadiliko yanaonekana katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, bila pesa wala chochote waheshimiwa wanajitolea hapa kwa usiku na mchana ili kuhakikisha mipango ya wananchi wetu inaenda sawa sawa.

Kamati ya Maji imezunguka katika Jimbo hili la Kilifi kuenda kuangalia kwa nini maji hayapatikani kule mashinani. Wamezunguka kwenda kukagua kila kitu. Leo wameweka *recommendations*; wameweka mambo ambayo kwamba yamepelekwa katika Idara husika ili tuhakikishe pande za Magarini, Gongoni na kila mahali kule maji yamewafikia wananchi. Huo ndio utendakazi wa Bunge hili. Tulitarajia sisi Seneta aje hapa atupatie maneno ya kutuunga mkono na kutuongeza nguvu. Amekuja kueleza maneno ambayo kwamba hayana msingi na hayakuturidhisha sana.

Mimi ombi langu ni kwamba, Seneta wetu tunamdai kuomba msamaha Bunge hili, kwa sababu Bunge hili ni Bunge la heshima na tumesimama kidete ili kuletea watu wetu wa Kilifi maendeleo. Na kama alikuwa anahitaji kuelimishwa ama kuelezewa mambo yanayoendelea Kilifi, angechukua muda wake na akaja akakaa na waheshimiwa. Ama akaenda akakaa na Idara husika zote, ili aelezewe ni nini na nini na mikakati gani inayoendelea kuliko kuja kujielezea vitu ambavyo ni mambo ambayo si ya ukweli. Mimi nataka kumalizia kwa kusema kwamba tunamdai hotuba ya kutuomba msamaha kama Bunge la Kilifi na wananchi wa Kilifi. Asante sana.

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Asante sana, mheshimiwa, kwa kutoa changizo zako kwa hotuba hii ya mheshimiwa wetu Seneta Stewart Madzayo. Bado nafasi iko kwa wale waheshimiwa ambao hawajapata fursa ya kuchangia hotuba hii maana tulikuwa tumesema kwamba wale wote ambao jana walichangia, kawaida huwa unachangia tu mara moja. Basi, waheshimiwa kwa sababu hakuna mheshimiwa yeyote ameweka *request* hapa, ningependa kuwapongeza nyote waheshimiwa wa jana na leo mliochangia hotuba hii.

ADJOURNMENT

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Temporary Speaker (Hon. Stephen): Kwa sababu hatuna la ziada, ningependa kuahirisha kikao hiki mpaka siku ya Jumatatu Mungu atakapotuajalia saa nane na nusu. Asanteni na muende nyumbani salama.

The House rose at 2:52 p.m.

Disclaimer*: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*